# **MUUNDO WA CHAMA (*AT-TAKATTUL AL-HIZBI*)**

Kutoka karne ya kumi na tatu hijriya (kumi na tisa miladiya) zimesimama harakati nyingi za mwamko (lakini) zikawa majaribio yasiofaulu hata kama zilibakisha athari ya kivitendo kwa wenye kuja baada yao ili kuregelea majaribio mara nyengine. Mwenye kufuatilia majaribio haya, mwanafunzi wa harakati hizi, ataona kwamba sababu misingi za kuangamia/ kuanguka/kutofaulu (*ikhfaq*) kwao huregelea kwa upande wa muundo kwa mambo manne:-

Ya kwanza—Zilikuwa zimebuniwa juu ya fikra jumla isiokuwa na mipaka, mpaka ikawa imefichika au yafanana na kufichika juu ya kwamba ilikuwa imepoteza (*tabalawara*), uweupe na usafi

.

Ya pili—Hawakujua twarika ya kutekeleza fikra zao, bali ikawa fikra yaenda kwa mbinu za kiholela na kikombo (*multawiya*), juu ya kwamba ilikuwa imezungukwa na kufichika na kutokuwa wazi.

Ya tatu—Walikuwa wakitegemea juu ya watu ambao haikukamilika ndani yake busara (*wa'iy*) sahihi, wala haikumakinika ndani yao niyya (*irada*) sahihi, bali walikuwa ni watu walio na hamu na hamasa tu.

Ya nne—Hawa watu waliochukua juu yao jukumu la harakati, hakukweko baina yao fungamano sahihi ila muundo tu iliochukuwa sura za vitendo na majina tofauti katika majina.

Kwa hivyo ilikuwa ni jambo la ki-maumbile kwamba kikundi hichi kikaripuka na kilichokuwa nayo ya hazina ya juhudi na hamasa mpaka wakakwishiwa na harakati yao ikapotea  na iliangamia na zikasimama baada yao harakati nyengine za watu wengine wakisimama na mzunguko huu huu hata wakakwishiwa na hazina yao na hamasa zao na juhudi zao kwa mipaka fulani na hivi hivi kuendelea.

Kuangamia harakati hizi zote ikawa ni jambo la ki-maumbile kwa sababu hazikusimama juu ya fikra sahihi wazi iliofungika na mipaka, wala hawakujua twarika ilionyoka, wala hazikusimama juu ya watu wenye busara wala juu ya fungamano sahihi.

Amma maudhui ya fikra na twarika, hino ni wazi katika makosa ya falsafa ambao harakai hizi zilisimama juu yake lau twafaridhisha kwamba walikuwa na falsafa. Hizi harakati zilikuwa harakati za Kiislamu na harakati za kikabila. Wasimamizi wa harakati za Kiislamu walikuwa wakilingania Uislamu kwa sura wazi pana, na walijaribu kufasiri Uislamu kwa tafsiri iliowafikiana na dhurufu zilizokweko wakati huo au waliotaka kuzichukua kutoka nidhamu nyengine mpaka Uislamu ufae kutabikishwa

juu yake na mpaka taawili hino iwe ni udhru kubakie kwake (nidhamu) au kuichukua. Amma wasimamizi wa harakati za kikabila, walikuwa waarabu miongozi mwao wakilingania kusimamishwa mwamko wa waarabu kwa msingi wa ukabila usiokuwa wazi wa kufichika pasina kujali Uislamu na Waislamu, na walikuwa wakitegemeo maneno ya ukabila, izza, karama, waarabu, uarabu, uhuru na yanayofanana nayo pasina maneno haya kuwa na mafhumu yeyote wazi kwao wao inayowafikiana na hakika ya mwamko. Na walikuwa maturuki miongoni mwao wakilingania kwa kusimamishwa mwamko wa biladi ya Turkiya kwa msingi wa ukabila, na walinganizi wa ukabila miongoni mwa waarabu na maturuki waliongozwa kwa mwongozo wa ukoloni ulioongoza pia Al-Balkan kwa hizi harakati za kikabila kuzitenganisha kwa uhuru kutokamana na serikali Uthmaniyya kwa sifa yake kama serikali ya Kiislamu.

Walisimama katika waarabu baina wanaume wa harakati mbali—za Kiislamu na za kikabila—mjadala wa maneno katika magazeti ya kawaida na magazeti jumla inayofupishwa kwa: Ipi ni bora na karibu zaidi, muungano wa kiarabu au muungano wa Kiislamu? Ikapita muda mrefu juhudi ikitumiwa juhudi ndani yake isiokuwa na natija kwa sababu kila mmoja katika muungano wa kiarabu na muungano wa Kiislamu hauna uhakika juu ya kwamba zilikuwa ni mipango ya kikoloni kutoa njiani akili na serikali ya Kiislamu. Kwa hivyo haikufupishwa kupoteza juhudi kwa kutokuwa na natija, bali ikapita haya na kuweka mbali serikali ya Kiislamu kutoka macho na akili.

Zikasimama kwa upande wa harakati za Kiislamu na harakati za kikabila harakati za kizalendo katika biladi tofauti za Kiislamu kama natija ya mkafiri mkoloni kuzichukua sehemu za serikali ya Kiislamu na natija ya dhulma za kisiasa na uchumi ziliotukia watu kwa ajili ya kutabikishwa nidhamu za kirasilmali juu yao. Juu ya kwamba harakati hizi zilikuwa na jibu kwa uchungu hu, baadhi zao zilibakia na upande wa Kiislamu ukiwatawala na miongoni mwao ukawa upande wa uzalendo ndio uliowatawala kwa ajili ya harakati za kutungwa alizozisimamisha mkoloni. Na kwa ajili ya upande huu wa kizalendo, hizi harakati zikaripuka na kushughulisha Umma na mapambano rahisi zilizothibitisha miguu ya maadui juu ya upungufu wao wa kutokweko na fikra yeyote ya kuzipeleka.

Sisi twaamani kwamba falsafa kweli ya mwamko ni mfumo unaojumuisha fikra na twarika pamoja, na kwamba mfumo huu ni Uislamu kwa sababu ni aqeeda inayotokamana kwayo nidhamu kwa mambo yote ya serikali na Ummah na kutatua kila tatizo la maisha. Pamoja na kuwa kwake nidhamu ya kiulimwengu, sio katika twarika

yake kuifanyia kazi kutoka mwanzo kwa sura ya kiulimwengu. Bali hakuna budi kuilingania kiulimwengu na kujaalia uwanja (*majal*) wa kuifanyia kazi katika eneo au maeneo mpaka imakinike ndani yake, isimame serikali ya Kiislamu ambayo itapunuka kimaumbile mpaka ikusanye biladi zote za Kiislamu mwanzo kasha ibebwe na serikali ya Kiislamu kwa yaliobakia katika upande wa ulimwengu kwa kuchukuliwa kwake kama ujumbe wake na kwa kuchukuliwa kwake kama ujumbe wa kibinadamu wa ki-ulimwengu wa kudumu. Ulimwengu mzima ni pahala pazuri kwa ulinganizi wa Kiislamu lakini kwa sababu watu wa biladi za Kiislamu wanaiamini Uislamu hakuna budi kwanza ulinganizi ndani yake. Na kwa sababu biladi za kiarabu kwa sifa zao kama biladi za Kiislamu zinazungumza lugha ya kiarabu na lugha ya kiarabu ni sehemu cha ki-msingi cha Uislamu na kiungo msini katika viungo vya thaqafa ya Kiislamu, ikawa biladi bora za kwanza kubeba ulinganizi huu ni biladi za kiarabu. Na hapana budi kukusanya pamoja uweza nguvu ya kiarabu na nguvu ya Uislamu ili kuunganisha lugha ya kiarabu na Uislamu kwa ajili yalio ndani mwao ya uweza wa kuathiri, kupanuka na kuenea. Kwa hivyo ni jambo la kimaumbile kuanza serikali ya Kiislamu katika biladi za kiarabu ili iwe kiini ya serikali ya Kiislamu itakayo kusanya biladi zote za Uislamu. Pamoja na kuwa ni lazima ulinganiwe Uislamu katika biladi za kiarabu, lakini pia ni lazima hivyo hivyo utumwe ulinganizi kwa biladi za Kiislamu zilizobakia. Sio maana ya kuanzia kazi katika biladi za kiarabu kwamba haifanywi kazi kwengine mpaka itimie kuziunganisha na serikali ya Kiislamu bali hufanywa kazi katika biladi za kiarabu ili kusimamisha serikali ya Kiislamu kasha serikali ipanuke kwa ujirani wake pasina kujali kuwa kwake biladi ya kiarabu au isiokuwa ya kiarabu.

Tumesema kwamba falsafa kweli ya mwamko ni mfumo unaojumuisha fikra na twarika pamoja. Na hakuna budi ila kufahamu hayo mawili kwa kila kikundi kinacholenga kutekeleza kazi yake kwa bidii itakayo fikisha kwa mwamko.

Mfumo huu umekuwa wazi na kufahamika kwake kwa ajili ya kikundi imekuwa rahisi. Basi ni jambo la kimaumbile kwamba baada ya ufafanuzi wa mfumo, kikundi kilichotanguliwa na ufahamu huu kuwa ni kundi cha kuathiri, hodari yenye kutangulia kinachostahiki mujtama kuilea na kuidhamini, na kubeba majukumu yake, kwa sababu ni kikundi kilichomeza fikra yake, chenye busara na twarika yake na chenye kufahamu qadhiya yake.

Lakini mujaradi tu ya kutanguliwa kwa ufahamu kwa kikundi haifikishi kwa mwamko sahihi mpaka ikiwa watu wafaa kwa kikundi hichi na ikiwa mfungamano ambao unawa fungamanisha watu hawa katika kuunda kikundi ni mfungamano sahihi unaozaa natija. Chama cha ki-mfumo

hufanya twarika ya mfungamano katika kikundi chake ni kuiamini aqeeda na kukhitimu katika thaqafa ya ki-chama. Kwa hivyo uamuzi kwa kufaa kwa watu kimaumbile kwa kuyayuka (*insihar*) kwao katika chama pindi ulinganizi unapoingiliana nao. Basi itakuwa kinachoamua kufaa kwao ni twarika ya mfungamano sio muundo wa chama kwa sababu kifungamano kinacho fungamanisha watu hawa katika kikundi ni aqeeda na thaqafa ya ki-chama kinachotokamana kutoka aqeeda hino.

Tukichunguza vikundi vilivyokweko katika harakati zilizodhihirika katika qarne zilizopita, tunaona kwamba twarika ya kuunda kwao fisidifu ikawa ni sababu msingi ya kuangamania kwao kwa sababu hazikubuniwa juu ya msingi wa kichama iliotanguliwa na ufahamu kweli bali zikasimama tu juu ya msingi wa mjumuiko au msingi wa chama jina. Hino ni kwa sababu walikuwa Waislamu kabla ya vita vya ulimwengu vya kwanza wakihisi kwamba wanao serikali ya Kiislamu. Pamoja na udhaifu ya serikali hino na kuangamia kwake, na tofauti wa mitazamo kwake, ilikuwa imechukua msingi wa mwelekeo wao wa kifikra na kimacho, waarabu wakiuona kuwa inameza haki zao na kuwapeleka kidikteta lakini walikuwa wakiielekea na macho yao na fahamu zao kwake ili kuisuluhisha kwa sababu ilikuwa serikali yao kwa hali zote. Hawa walikuwa na upungufu katika kufahamu hakika ya mwamko na kufahamu twarika yake, na haikupatikana kikundi miongoni mwao. Twaweza kuhukumu kwamba hawa walikuwa aghlabu ya Waislamu.

Lakini katika wakati huu ilikuwa thaqafa ya kigeni imevamia biladi za Kiislamu na kwa kupitia kwake wakoloni wakaweza kuvutia kwao kipote cha Waislamu walio wachochea kusimamisha vikundi vya kichama ndani ya serikali ya Kiislamu zilizosimama juu ya msingi wa utengamano na uhuru. Na wakaloni wakaweza kwa sura khasa kuwavutia kwao wao kipote cha waarabu walio wakusanya Paris ili kutengeneza kutoka kwao kundi kinachosimama kuipiga vita serikali ya ki-Uthmani kwa jina la uhuru wa waarabu kutoka kwake. Hino thaqafa ndio iliowajumuisha pamoja na fikra geni na hisia za uzalendo na ukabila alizoziunda mkafiri mkoloni ndani yao. Ikawa mfungamano wao wa ki-akili na hisia moja na mantiki moja iliwajumuisha iliofikisha kwa kuunganisha lengo nayo ni uhuru wa taifa la kiarabu maadamu serikali Uthmaniya inadharau maslahi zao na ikajiruhusu nafsi yake kuwadhulumu na kula haki zao. Ikawa lengo hino ya muungano ni mbinu ya kuunda juu yake kikundi cha chama jina iliofikisha kwa kuandaa mapinduzi ya kiarabu na kuzaa natija iliozaa ya kueneza athari (*nufudh*) ya ukafiri na ukoloni juu ya biladi za Kiislamu na makhsusan biladi za kiarabu. Kazi za vyama hivi vikamalizika kwa mpaka huu na wakagawanya ngawira kwa kuwa kwao viongozi wa baadhi ya biladi za Kiislamu kama vibaraka wa ukoloni huu.

Baada ilipoondosha serikali ya Kiislamu kutoka kuwepo maishani, ukoloni ukasimama pahala pake ikihukumu biladi za kiarabu moja kwa moja na kueneza athari yake kwa yaliobakia katika biladi za Kiislamu. Waliingia biladi za kiarabu kivitendo na wakachukua kumakinisha miguu katika kila sehemu zake kwa mbinu na njia zake chafu za kufichika ambayo katika muhimu miongoni zake ni thaqafa ya ukoloni geni, mali na vibaraka.

Thaqafa geni ilikuwa na athari kubwa katika kumakinisha ukafiri na ukoloni katika kutofaulu mwambo na kuangamia kila harakati ya kikundi sawa sawa iwe ya kijumuiyya au ya kichama kwa sababu thaqafa ina athari kubwa juu ya fikra ya kibinadamu ambayo inaathiri mwenedeo ya uhai. Ukoloni uliweka manhaj ya masomo na thaqafa juuy a msingi wa falsafa thabiti nayo ni mtazamo katika uhai ambayo ni kutenganisha mada na roho na kutenganisha dini ya serikali. Ukafanya shaksiyya yake peke yake kuwa ni msingi ambayo kuchukua kutokamana kwayo thaqafa yetu. Na ukafanya hadhara yake na viungo (*mukawwinat*) vya biladi yake na tarekhe yake na mazingara yake ni nukta ya kuanza ya msingi tunayojaza nayo akili zetu.Wala haukutosheka na hayo, bali pia ukafanya makosa maksudi katika ilichonyang’anya kutoka kwetu kutoka shaksiyya yake kutoka fahamu ya uhakika na ukageuza sura ya ukoloni juu ya shaksiyya hino kwa kuipa pahala bora ambayo huigizwa na pahala penye nguvu. Kisha ukaingia katika ufafanuzi wa mpango (*baramij*) mpaka isitoke sehemu moja kutoka hino manhaj jumla. Kwa hivyo tukawa twasomeshwa thaqafa fisidifu inayotufundisha vipi wengine hufikiri, na ikatufanya hatuwezi—kimaumbile—kutojua vipi tunavyofikiri sisi kwa sababu fikra yetu haihusiki na mazingara yetu, shaksiyya yetu na tarekhe yetu wala (*mustamad*) kutokamana na mfumo wetu. Basi tukawa—kwa sifa yetu kama wasomi—wageni na watu, tusiofahamu mazingara yetu wala mahitaji yake. Kwa hivyo ikawa hisia za wasomi zimetengwa na fikra zao na akili zao na ikawa fikra hino—kimaumbile—haifikisha kwa kufahamu kisawa hali iliosimama katika biladi wala haifikishi kwa kufahamu mahitaji ya Ummah wala haifikishi kwa ufahamu mzuri wa twarika ya mwamko kwa sababu ilikuwa fikra iliotengwa na hisia lau kama haikuwa tupu na hisia. Na juu ya hayo yote ilikuwa fikra geni inayobebwa mtu aliye na hisia za Kiislamu. Fikra hino kawa kimaumbile haifikishi kwa kikundi sahihi iliotanguliwa na fahamu sahihi. Wala athari ya thaqafa geni haikusimama kwa wasomi peke yao bali ikawa fikra ya mujtama mzima kwa ajili ya fikra iliobebwa na thaqafa hino imetengwa na hisia yake, na ikawa kwa sababu hino matatizo ikazidisha katika mujtama na ikazidi mzigo wa mwamko juu ya kikundi cha kichama sahihi juu ya yaliyokweko kabla ya vita vya ulimwengu wa kwanzo. Kwa sababu baada kuwa tatizo iliokabili Ummah au chama ni tatizo la

mwamko katika mujtama wa Kiislamu ikawa tatizo sasa ni kuzalisha masikizano (*tanasuq*) baina watu binafsi wa mujtama na jamii zao katika fikra na hisia mahsusan baina wasomi na mujtama yao kwa sababu hawa wasomi walikuwa wamejitolea kikweli kwa fikra geni tu, kando na hisia, na kujitolea hivi ukawapeleka kuwa wageni na mujtama wao na kuupuza, kutengamana nayo na kuukabili na kutojali kama ulivowapeleka kuwa rafiki na mgeni, kumtukuza, kujikurubisha kwake na kumkabili na hamu hata kama alikuwa mkoloni. Kwa hivyo haiwezekani kwa msomi huyu kuwazia dhurufu zilizoko katika biladi yake ila kwa kumwigiza mgeni katika kuwazia dhurufu za biladi yake pasina kufahamu hakika ya dhurufu hizi; basi akawa hajui kitakacholeta mwamko kwa Ummah ila kwa kumwigiza mgeni pindi anapozungumza juu ya miamko. Wala hisia za msomi huyu hazikuchangamka kwa ajili ya mfumo bali zilichangama tu kwa ajili ya biladi na watu na hino ni mchangamko wa kimakosa. Pamoja na hayo, hakusimama kwa mapinduzi msimamo wa kweli wala hakujitolea kwa ajili ya watu kujitolea kamili wala hakuhisi hisia za kifikra juu ya dhurufu zilizomzingira wala kuhisi hisia za kifikra mahitaji ya watu. Hata tukisema alisimama kwa mapinduzi na kutafuta mwamko, ikawa ni msimamo ambayo ni matunda ya mgongano na maslahi yake khasa au msimamo wa kuigiza mapinduzi ya watu. Kwa hivyo haikuchelewa kupotea pindi ilipomalizika mgongono kwa kumpa kazi au kuridhisha mwelekeo wake au kupotea pindi ilipogongana na uchoyo wake na manufaa yake au alipopatikana na maudhia.

Mfano wa huyu hauwezekani kupatikana kikundi sahihi kutokamana kwake mpaka atibiwe kwa kuleta muungano baina fikra yake na hisia zake kwa kumsomesha upya thaqafa sahihi ya kimfumo yaani thaqafa ya Kiislamu. Na kumtibu na thaqafa hino hulazimisha kumfanya mwanafunzi anayeundwa akili yake muundo mpya mpaka igure baada kutatua tatizo hino kwa kuleta muungano baina yake na mujtama wake ili isahilike wakati huo kutatua tatizo la mwamko katika mujtama. Lau si thaqafa geni ingelikuwa mwamko ni kazi ndogo kuliko ilivyoko leo.

Kwa hivyo ni muhali kuwepo kikundi cha kichama sahihi katika mujtama na hino thaqafa geni, wala kuwepo juu ya msingi wake mfano wa kikundi hichi.

Wala ukoloni haikusimama kwa thaqafa huu bali ukatia sumu kwa mazingara kwa fikra, rai, siasa na falsafa uliofisidisha nazo mazingara ya Kiislamu na kuchanganyisha kiwazi fikra za Waislamu katika upande tofauti za kimaisha. Kwa hayo ikapotea kwao msingi inaozunguka juu yake kuamka kwao wa kimaumbile na ukafanya kila mwako kubadilika harakati ya kimchanganyiko wa kimgongano inayofanana na harakati ya aliyechinjwa inayomalizika kwa kupotea, kukata tamaa na kusalimu amri.

Mgeni alitumia kufanya shakhsiyya yake msingi wa mzunguko wa thaqafa na kituo cha kuelekea kwake— akaitumia katika upande za kisiasa, na akafanya qibla cha wanasiasa au wanasiasa kikazi ni kutafuta usaidizi kwa mgeni na kumtegemea. Kwa hivyo zikawa vikundi vingi vikijaribu—pasina kuhisi—kutafuta usaidizi kwa wageni. Wakasimama katika biladi walioona ni sawa kutafuta usaidizi kwa serikali geni pasina kufahamu kwamba kila kutafuta usaidizi kwa mgeni na kulingania kumtegemea mgeni—pasina kujali jinsi yake—huhisabiwa kuwa ni sumu ya kigeni na khiyana kwa Umma hata ikiwa kwa nia nzuri. Wakawa hawafahamu kwamba kuunganisha qadhiya yetu na wasiokuwa sisi huhisibiwa kuwa kujiuwa kisiasa. Kwa hivyo haimkiniki kufaulu kwa kusimama kikundi chechote kilichotiwa sumu fikra yake na kumtegemea mgeni au kulingania kwake.

Kadhalika walitumia sumu katika mazingara ya uzalendo, ukabila na ujamaa kama walivyoitia sumu ya uzalendo wa eneo finyo (*al-iqlimiyya ad-dhayiqqa*) na kuifanya kuwa ni kiini cha kazi ya kileo; kama ilivyoitia sumu tena ya kutowezekana kusimama serikali ya Kiislamu na kutowezekana kuungana biladi za Kiislamu pamoja na kuweko tofauti za kimiji, rangi na lugha juu ya kwamba wote ni Umma mmoja waliofungamishwa na aqeeda ya Kiislamu inayotokamana kwayo nidhamu yake. Na ikaitia sumu na mengineo pia miongoni mwa fikra za kisiasa za kimakosa kwa mfano msemo wao: “Chukua kisha uombe” na: “Ummah ni chimbuko la nguvu za utawala” na: “Ubwana ni kwa watu” na nyenginezo. Na ikaitia sumu na fikra za kimakosa kwa mfano msemo wao: “Nchi ni juu ya wote” na: “Izza ni kwa nchi” na yanayofanana nayo. Na kadhalika ikaitia sumu na rai za kufuatana na kupelekwa na mazingara kwa mfano msemo wao: “Sisi twachukua nidhamu yetu kutoka mazingara yetu” na: “Kuridhika na amri ilioko” na: “Lazima tuwe wenye kulingana na mazingara” na yanayofanana nayo.

Ikawa matunda ya sumu hizi ni kusimama katika biladi za Kiislamu, na miongoni mwao biladi za kiarabu, hali isiofikisha kwa kusimama kikundi sahihi. Kwa hivyo si ajabu kuangamia vikundi vyote vya kichama jina, kwa sababu hazikusimama juu ya msinga wa fikra pana inaofikisha kwa mpangilio makini na uandazi wa kuaminiwa bali zikasimama pasina msingi.

Kwa hivyo ikawa ni kimaumbile kwa zile vyama vilivyosimama katika ulimwengu wa Kiislamu, na makhsusan ulimwengu wa kiarabu, kuwa vyama vyenye migongano kindani (*mufakkak*) kwa sababu zilisimama pasina mfumo. Na mwenye kuvifuatilia huona kwamba vilisimama juu ya msingi wa matukio yaliotokea yalioleta dhurufu zilizolazimisha kusimama vikundi vya kichama, kisha zikamalizika hizo dhurufu na

zikamalizika vyama kwa kumalizika kwake au zikadhoofika na kupotea. Au zikasimama juu ya msingi wa urafiki baina watu walioletwa pamoja kwa urafiki huu basi wakasimamisha kikundi kwa msingi wake, na zikamalizika kwa kuzunguka kwao juu ya nafsi zao wenyewe. Au juu ya msingi ya maslahi ya kisasa ya kibinafsi au mengineo. Kwa hivyo haikweko baina watu waliofanya kikundi juu ya msingi hizi, na katika mazingara na mijtamaa haya, mfungamano wa kichama wa kimfumo. Basi ikawa kuweko kwao si tupu na manufaa tu basli madhara kwa Umma. Juu ya kuwa kuwepo kwao katika mujtama ilikuwa kizuizi kuwepo uchama sahihi au kuakhirisha kuwepo kwake, zilipanda katika nafsi za wengi na kujaza katika nyoyo za jumla ya watu giza na shaka, na kusababisha wasiwasi katika kila harakati ya kichama hata ikiwa sahihi. Zikapanda katika watu chuki za kibinafsi na chuki za kiukoo, na zikawafunza kwa mbinu zake kutokuwa na msimamo na mzunguko nyuma ya manufaa. Kwa maana nyengine walifisidisha maumbile masafi katika wengi wa watu na kuzidisha mzigo mzito juu ya vikundi vya kichama sahihi ambavyo havina budi kutokamana na katikati ya aghlabu ya watu.

Zikasimama kwa upande wa harakati za Kiislamu, ukabila na uzalendo harakati za kiujamaa zilizosimama juu ya msingi wa kimada. Zikawa harakati hizi zafuata harakati ya kiujamaa katika urusi na kuongozwa na mwongozo wake, na twarika zao ikawa ni uvundifu na uharibifu. Lengo zao—juu ya kuleta ujamaa katika biladi—ni kuchanganyisha ukoloni wa kimagharibi kwa maslahi ya kambi ya kimashariki kwa sifa ya kuwa wasimamizi wao walikuwa ni vibaraka kwake. Hizi harakati hazikusikizana na Umma wala kuleta athari; na ikawa kuangamia kwao ni kimaumbile kwa sababu zinagongana na maumbile ya mwanadamu na kugongana na aqeeda ya Kiislamu. Zilitumia uzalendo kwa shabaha zao, na zikawa ni tatizo juu ya matatizo inayogandamizwa chini yake mujtamaa.

Na zikasimama vikundi vyengine juu ya msingi wa ujumuiyya. Zikasimama katika biladi jumuiyya za kikaribu (*mahaliyya*) na kieneo zikilenga kwa malengo ya kikheri. Zikasimamisha madrasa, mahospitali na majumba ya ukimbizi (*malaji*), na zikasaidia katika vitendo vya uwema na uzuri. Na ikawa athari ya kitaifa zikizidi katika jumuiyya hizi. Ukoloni ilishajiisha jumuiyya hizi mpaka zikadhihirisha vitendo vyake vya ukheri kwa watu. Na zikawa nyingi ni jumuiyya za kithaqafa na ukheri wala haikupatikana jumuiyya ya kisiasa ila kwa uchache.

Ikitizamwa kwa jicho makini kwa natija za jumuiyya hizi, inaonekana kuwa hazikuzalisha chochote cha kunufaisha Umma au kusaidia kwa mwamko. Na madhara zao zikawa za kufichika pasina kudhihirika ila

kwa mwenye umakini, pamoja na kuwa kuwepo kwao kwa msingi wake ni madhara makubwa bila kupima manufaa ya kisehemu. Hino ni kwa sababu Umma ya Kiislamu kwa uzima wake, kwa hukmu ya kuwepo baadhi za fikra za Kiislamu, na kwa hukmu na kutabikisha kwake baadhi ya hukmu za ki-Sheria, na kwa hukmu ya kumakinika hisia za Kiislamu ndani yake kwa athari ya Uislamu, huwepo ndani yake hisia za mwamko na ipo ndani yake hamasa ya kheri na mwelekeo wa kimaumbile wa ukikundi, kwa sababu roho ya Uislamu ni roho ya kijamaa. Basi ikiwachwa Umma ya Kiislamu na jambo lake, itabadilika hisia hino—kimantiqi—kuwa fikra, na fikra hino itazalisha kitendo cha kuendeleza Umma. Lakini kuwepo jumuiyya huzuia haya kwa sababu zikawa ni kutoa pumzi kwa hamasa hino ya moto na kuzitumia hisia hizi kwa sehemu hino ya kitendo ambayo ni sehemu ya kijumuiyya. Basi aliono mwanachama wa jumuiyya kwamba amejenga madrasa au kusimamisha hospitali au kushiriki kwa amali njema basi huhisi raha na utulivu na kukinaika na amali hino. Ilhali lau asingelisimamisha jumuiyya hino, roho ya ujumuiyya ingelimsukumu kwa kikundi sahihi nayo ni kikundi cha kichama ambayo italeta mwamko sahihi.

Zikasimama kwa upande wa jumuiyya za kithaqafa na kheri jumuiyya za kiakhlaqi zilizofanya kazi kuendeleza Ummah kwa msingi wa akhlaqi kupitia waadhi na nasiha, mihadhara na matoleo, kwa kuhisabu ya kwamba akhlaqi ndio msingi wa maendeleo. Hizi jumuiyya zilijitolea kijuhudi na kimali lakini hazikuwa na natija muhimu. Walizitoa hamasa za Ummah kwa mazungumzo haya ya kikawaida ya kuregelewa yasiochangamsha. Mfano wa jumuiyya hizi zilisimamisha juu ya fahamu ya makosa ya msemo wake *ta'ala* akimkhutubia Mtume (saaw):

**وإنك لعلى خلق عظيم {القلم :4}**

"*Hakika wewe una akhlaqi njema kabisa*" [Al-Qalam:4] juu ya kwamba hino ni sifa ya shaksiyya ya Mtume si wa mujtama. Na wa msemo wake (saaw): "Hakika Allah amenituma nitimize akhlaqi za hali ya juu" na msemo wake (saaw): "Hakika nimetumwa kutimiza akhlaqi za hali ya juu" juu ya kwamba hadithi hizi mbili na mifano yake zinahusika na sifa za mtu binafsi si jamii. Na zilijengwa juu ya kosa la mshairi katika msemo wake:

Hakika Umma ni akhlaqi zikibakia Na zikipotea akhlaqi zao wao hupotea.

Juu ya kwamba Umma haziwi kwa akhlaqi bali huwa kwa aqeeda wanazoziamini, fikra wanazozibeba na nidhamu wanazotabikisha. Pia zilikuwa zilibuniwa juu ya fahamu makosa kwa maana ya mujtama ya kwamba huundwa na watu binafsi ilhali hakika mujtama ni mjumuiko ilioundwa na sehemu ambazo ni: Watu, fikra, hisia na nidhamu.

Kufisidika kwake hutokea kwa kufisidika fikra, hisia na nidhamu si kwa kufisidika watu. Na kusulihika kwake huwa kwa kusuluhika kwa fikra, hisia na nidhamu zake.

Kadhalika zikawa zimebuniwa juu ya yaliomakinika katika mabongo ya wengi wa wenye kusuluhisha na wanavyuoni wa akhlaqi ya kuwa jamii huharibiwa na mtu binafsi, na mtu binafsi hujengwa na kuharibiwa na akhlaqi zake. Basi akhlaqi za kunyoka humfanya mwenye nguvu, mwenye kunyoka, mwenye athari, mwenye kuzaa natija, mtendaji kheri na uwema na mwenye kusuluhisha. Amma akhlaqi mbaya humfanya dhaifu, mlegevu, pasina manufaa wala kheri, pasina hamu katika maisha ila kushibisha matamanio yake na kuridhisha uchoyo wake. Kwa hivyo waliona kwamba kusuluhisha jamaa yaja tu kwa twarika ya kumsuluhisha mtu binafsi, basi walilenga kusuluhisha mujtama kwa manhaj ya akhlaqi wakifauli kupitia kwa akhlaqi kuendeleza Umma.

Juu ya kuangamia kila harakati ya kusuluhisha iliosimama kwa msingi wa qaida ya akhlaqi, watu hawawachi kukinai kwamba qaida hino ndio msingi wa kusuluhisha, na wakasimamisha jumuiyya za kusuluhisha kwa msingi huu. Ilhali hakika ni kwamba mbinu za kusuluhisha jamii sizo mbinu za kumsuluhisha mtu binafsi hata kama yeye ni sehemu ya jamii, kwa sababu ufisadi wa jamii hutokea kwa kufisidika hisia zake za kijamii, na kufisidika kwa mazingara yake ya kifikra na kiroho. Na hutokea pia kwa kuweko fahamu makosa katika jamii. Kwa maana nyengine, hutokea kwa kwa kufisidika mazowea (*‘urf*) jumla. Kusuluhika kwake haitokei ila kwa kuunda mazowea jumla mazuri, au kwa maana nyengine haitokei ili kwa kusuluhisha hisia za kijamii, na kuunda mazingara sahihi ya kiroho na mazingara ya kifikra yanaohusika na upande wa kiroho, na kutabakisha nidhamu kutokamana na serikali. Wala hino haitokei ila kwa kuunda mazingara ya Kiislamu, na hakuna budi ila kusahihisha fahamu za vitu kwa watu wote. Na hino haitokei kupitia kikundi juu ya msingi wa kijumuiyya, wala kufanya akhlaqi, waadhi na nasiha kuwa msingi wa kikundi.

Kutokamana hapa ikaja kuangamia kila kikundi kwa msingi wa kijumuiyya katika kuleta mwamko au kusuluhisha, kama ilivyokuja kuangamia kila kikundi kwa msingi wa chama jina ambayo haikubuniwa juu ya mfumo maalumu wala haikutanguliwa na fahamu yeyote wala haikufanya mfungamano wake kubuniwa juu ya muungano sahihi baina ya watu binafsi.

Na ikawa kuangamia vikundi vyote pia ilihakikishwa katika upande wa watu binafsi kwa sababu juu ya kusimama kwao kwa msingi usiokuwa wa kikundi sahihi kwa kutokweko fikra na twarika, na makosa ya twarika katika kikundi, ukikundi wao haukusimama juu ya kufaa mtu binafsi

mwenyewe bali ukasimama juu ya msingi wa nafasi yake katika mujtama na uwezekano wa kuwepo faida ya haraka kwa kuwa kwake katika chama au jumuiyya.

Mwanachama alikuwa akichaguliwa kwa msingi ya kuwa yeye ni mwenye uso katika watu wake au tajiri katika jamii zake au wakili, daktari au mwenye nafasi na nguvu pasina kujali kufaa kwake kwa kikundi hichi anacho chaguliwa au asifae. Kwa hivyo ilizidi katika vikundi utengamano baina wanavyama wao kama ilivyozidi upande wa kitabaka. Iliingia katika wanachama wa chama au jumuiyya hisia ya kufichika kwambo wao wana ubora juu ya watu waliobakia, si kwa mali zao na nyuso zao tu, bali kwa kuwa kwao wanachama katika chama au jumuiyya. Kwa hivyo haikutokea baina yao na watu maingiliano au makurubiano yeyote basi ikawa kuwepo jumuiyya au chama balaa juu ya balaa na tatizo mpya juu ya matatizo iliozama chini yake mujtuma huu.

Kwa hivyo twaweza kusema baada kusoma, kufikiri na kuchunguza kwamba haikutokea katika biladi zote za Kiislamu katika karne zilizopita kikundi chochote sahihi itakayo fikisha kwa mwamko. Vikundi vyote zilizotokea ziliangamia kwa kusimama kwao juu ya msingi wa makosa pamoja na kuwa Umma haitosimama ila kwa kikundi. Basi ni kikundi gani sahihi kitakayo sababisha mwamko wa Umma? Hino ndio tunayohitaji kubainisha.

Kikundi sahihi ambayo kupitika kwake Umma itaendelea haijuzu kuwa kwa msingi wa kijumuiyya ambayo hulazimika na nidhamu yake ya kijumuiyya kutenda vitendo na misemo au vitendo tu au misemo tu. Kikundi sampuli hino haijuzu kushajiishwa katika Umma inayopenda mwamko, wala haijuzu kuwepo juu ya msingi wa vyama visiokuwa vya kimfumo kama zilizosimama katika ulimwengu wa Kiislamu kutoka vita vya ulimwengu wa kwanza mpaka leo.

Kikundi sahihi ni kile kinachosimama juu ya msingi wa Kiislamu wa kimfumo ikiwa fikra ndio roho ya mwili wa chama, nayo ni kiini chake na siri ya uhai wake. Na kitakuwa kiini cha kwanza ni mtu inayojaa ndani yake fikra na twarika kwa jinsi yakempaka atakuwa mtu huyu jinsi ya fikra katika uweupe na usafi wake, na mfano wa twarika katika katika uwazi wake na kunyoka kwake. Pindi panapo kwepo vitu hivi vitatu: Fikra pana, twarika wazi na mtu msafi, imepatikana kiini cha kwanza. Kisha hakitochelewa kiini hichi kuzidi kuwa viini vitakavyo kuwa halaqa ya kwanza ya chama (uongozi wa chama). Pindi panapo kwepo halaqa ya kwanza basi pamepandwa kikundi cha kichama kwa sababu halaqa hino haitochelewa kubadilika kuwa ni kikundi. Na hapo kikundi hichi kitahitaji mfungamano wa kichama, kinacho jumuisha baina ya watu wanaoamini fikra na twarika. Hino fungamano ya kichama ndio aqeeda

inayotokamana kwayo falsafa ya chama na thaqafa kwa fahamu zake huitwa chama. Hapo itakuwa kikundi cha kichama kime undwa na kitasongea katika ukweli wa maisha. Itakabiliwa na mazingara ya moto na baridi, na kitavumiwa na upepo mkali na laini, na kitazungukiwa na hewa ya mawingo na safi; kikiweza kusimama imara kwa mambo haya basi fikra yake itakuwa imefafanulika, twarika yake kuwa wazi, kutayarishwa watu wake na mfungamano wake kuwa na nguvu. Na kitaweza kupiga khatua ya kivitendo katika da'wah na kitendo kutoka kikundi cha kichama kuwa chama cha kimfumo kamili inayofanyia kazi mwamko kweli. Hino ndio kikundi sahihi ambacho kiini chake ni fikra kwa sababu huwo ndio msingi wa uhai.

Amma vipi itatokea kikundi hichi cha kichama cha kimfumo katika Umma inayotaka mwamko kimaumbile, hino ndio ufafanuzi:-

Umma ni mwili mmoja usiotengana, na kwa muundo wake kamili ni kama mwanadamu. Kama mwanadamu akiugua maradhi makali inayomkurubisha kwa kifo kisha huanza uhai kuenea ndani yake basi huenea ndani yake kwa ukamilifu wake kwa sifa yake kamili, kadhalika Ummah iliodidimia huchukuliwa kuwa mgonja. Na pindi inapoenea uhai ndani yake huenea katika mjumuiko wake kwa sifa yake kama mkusanyiko ya mtu mmoja kwa kuchukuliwa kwake kwa ukamilifu. Uhai kwa Ummah ni fikra inayosuhubiwa na twarika katika jinsi yake ili kutekelezwa nayo; na mjumuiko wake huitwa mfumo.

Na haitoshi mujaradi ya kuwepo tu mfumo katika Ummah kuhuisha uhai ndani yake bali kuongozwa kwake kwa mfumo na kuiweka pahala pa kuitekeleza katika uhai wake ndio inayoijaalia kuwa uhai kwa sababu mfumo yaweza kuwepo katika Ummah katika mirathi yake ya kiSheria, thaqafa na tarekhe lakini imeghafilika nayo au kughafilika na fikra yake na twarika yake, au kughafilika na kuunganisha baina yao pamoja. Basi katika hali hii, kuwepo tu fikra na twarika haitofikisha kwa mwamko.

Uhai huenea kikawaida katika Umma inapotokea mitetemeko mizito katika mujtama inayozalisha hisia za kushirikiwa pamoja. Hisia hizi za kijamii hufikisha kwa amaliyya ya fikra inayozaa natija ya maqadhiya kupitia uchunguzi katika sababu na yaliosababishwa na mitetemeko haya, na mbinu za karibu na za mbali zitakao okoa kwayo. Ila hizi hisia hata kama ni mmoja na za kushirikiwa katika jamii baina watu wake binafsi, zitakuwa kwa nisabu tofauti baina ya watu kwa kiwango aliowatayarisha nayo Allah kwa aliowatunuku ya matayarisho ya kipwekee. Kwa hivyo itabakia kuongoka kwake kwa fikra itakuwa imefichika ndani yake mpaka ijumuike taathira yake na imakinike katika wale walionali uweza mkubwa katika hisia ili iwaamshe, kuwaongoza na kuamsha ndani yao harakati mpaka zidhihirike dalili za uhai ndani yao mwanzo.

Hawa walionali uweza mkubwa wa hisia imechapishwa ndani yao kimaumbile ndani yao hisia za kijamii na itamikinika fikra ndani yao mpaka watachangamka na harakati ya busara na ufahamu, na wao ni macho ya Umma na kipote chenye busara ndani yao.

Lakini kipote hichi chenye busara kitachanganyikiwa na kuwa na tahayari kikiona njia nyingi kikitahayarika juu ya njia ya kufuata. Lakini harakati hino ya busara katika kipote cha jamii kitatofautika nisabu yake ndani yake. Mantiki ya hisia katika baadhi yao itakuwa kubwa zaidi kuliko baadhi wengine basi kitasimama kikosi kipwekee baina kipote hichi chenye busara kitakacho chagua njia katika njia baada darasa na kumakinika katika usomi, kikifahamu lengo itakacho fikia kama kinavyofahamu uwazi wa njia na kuifuata na kuenda kwa njia ya lengo lake. Kwa hivyo kitaongoka kwa mfumo kwa fikra na twarika yake na kuamini aqeeda ya kimakinika itakayo waingilia kiwiliwili ili iwe aqeeda yao. Aqeeda pamoja na thaqafa ya chama itakuwa ni mfungamano baina watu katika kikosi hichi.

Pindi mfumo inapoingia kiwiliwili katika watu, haiwezi kubakia mahbusu bali itawasukuma kwa kulingania kwake. Vitendo vyao zitaundwa nayo zikipelekwa kwa mujibu ya manhaj yake, zikifungwa na mipaka yake, na kuwepo kwao itakuwa kwa ajili ya mfumo na kwa ajili ya kulingania kwake na kutekeleza majukumu yake. Ulinganizi huu utalenga kuwakinaisha watu mfumo kipekee si nyengine, na kwa kuunda wai amma ndani yake. Halaqa ya kwanza itabadilika kuwa kikundi (*kutla*) kisha kitabadilika kikundi kuwa ni kikundi cha kichama (*kutla hizbiyya*) itakayo kuwa kimaumbile katika upande mbili; moja wapo ni kuzidi katika viini vyake kwa kuunda viini vipya wanaoamini mfumo kwa busara na ufahamu wa kuaminika, na ya pili yao kwa kuunda wai amma juu yake katika Ummah jumla. Wai hino amma juu ya mfumo itafanya fikra, rai na aqeeda katika Ummah, muungano wa kijamii kama haitokuwa muungano wa wote. Kwa hayo lengo la Ummah itakuwa moja, na aqeeda yao na mtazamo wao kimaisha itakuwa moja. Kwa hivyo chama itakuwa ni (*butaqa*) inayo yayusha Ummah na kuisafisha kutoka uchafu na ufisadi ziliofikisha kwa kudidimia kwake au yaliyozalishwa katika udidimizi wake. Chama itasimamia amali hino ya kuyayusha katika Umma na ndio itakayo sababisha mwamko, na ni amali nzito. Kwa hivyo haitoiweza ila chama inayoishi fikra yake na kuifanya uhai wake kusimama juu yake, na kufahamu kila khatua katika khatua zake.

Hino ni kwa sababu hisia inayofikisha kwa fikra ndani ya chama, fikra hino itang'ara katika Ummah baina fikra nyingi na itakuwa moja wapo. Mwanzo wake itakua dhaifu kwa sababu ni changa zaidi kuzaliwa na kuundwa, baada haijamakinika wala kuwa na mazingara; lakini kwa

sababu fikra ni natija na mantiki ya hisia yaani ufahamu natija ya ufahamu wa kihisia basi itazalisha hisia ya kifikra yaani hisia wazi natija ya fikra ya kindani. Basi itasafisha, kimaumbile, kila mwenye kuathirika nayo na kumfanya mukhlis hata asitake kuwa mukhlis hatoweza. Na itamwingilia kiwiliwili mukhlis fikra hino, aqeeda na thaqafa, mpaka izalishe ndani yake mwamko usiofungika ndani yake. Na mwamko hu si chochote ila mripuko baada kuchomeka katika hisia na fikra inayoeneza katika ulinganizi moto, hamasa na ukweli kama inavyoeneza ndani yake—wakati huo huo—mantiki na fikra. Itakuwa moto unaochoma ufisadi na mwangaza unaoangaza njia ya ubora. Kwa haya ulinganizi itatukia katika mvutano na fikra fisidifu, aqeeda didimizi na mazowea ya kibalaa ambazo zitajaribu kujitetea lakini kujitetea yenyewe itakua ni kusuguliwa pamoja (*ihtikak*) na mfumo mpya inayozidisha nguvu yake. Mvutano huu utaendelea mpaka zitadidimia kila fikra, aqeeda na njia na kubakia mfumo wa chama pekee katika Umma kuwa fikra yake na aqeeda yake.

Pindi chama kinapounda fikra, aqeeda na rai basi itakuwa imefanya kuunganisha Umma kwa busara makini, kuiyayusha na kuisafisha mpaka itakuwa Umma mmoja; kwa itakuwepo umoja sahihi.

Kisha itakuja marhala ya pili ya chama, nayo ni kuongoza Umma kutekeleza amali ya kurekebisha kimapinduzi ili kuamsha Ummah kisha kubeba pamoja ujumbe wa Uislamu kwa watu na umma nyenginezo ili kutekeleza jukumu lake kwa wanadamu.

Hichi kikundi cha kichama ni kikundi cha kijamii wala haimkiniki ila kuwa harakati ya kijamii kwa sababu kikundi sahihi haiwi harakati ya kibinafsi. Kwa hivyo ni lazima juu ya wasimamizi wa chama katika biladi za Kiislamu kusoma usomi fafanuzi juu ya vikundi vya kijamii na kuzifahamu ufahamu wa kindani.

Ufahamu wa harakati za kijamii zilio na nguvu ya kuathiri katika wakati wake hutuonyesha kwamba haziundwi inapo kuwepo starehe rahisi, haki za kikawaida kwa watu zimehakikishwa, kupatikana maisha mazuri na inapokuwa kufaa mtu ndio kipimo cha kutawala mambo muhimu. Fahamu hino ya harakati za kijamii inatusahilishia kupima kila harakati ya kijamii kwa mizani yake sawa kwa kusoma mazingara ilioishi au inayoishi ndani yake harakati na dhurufu zilizo au zinazo zienea, na nafasi ya kazi ya watu wahodari katika kupeleka mambo yake na kusahilisha majukumu yake kuvunja yanayo zuia au kuchelewesha kufaulu kwake.

Na hupimwa kufaulu kwake kwa uweza wake kuchangamsha moyo wa kukasirika katika watu na kuwashajiisha kudhihirisha hasira zao kila

inapotokea utawala inayotawala au nidhamu iliopo kwenda kinyume na mfumo huu wao au kuhukumu juu yao kulingana na maslahi ya utawala na hawa yake.

Ufahamu wa harakati hizi za kijamii hutulazimisha kusoma maisha katika mujtama, maarifa ya mahusiano ya Ummah na viongozi wake, na mahusiano ya viongozi hawa na Ummah, nguvu ya kila moja katika hizi na hakika yake kamili kwa mtazamo wa Uislamu na rai, fikra na hukmu inazozilangania. Na kipimo cha ilivyoko mujtama, na inayo (*'aradhat lahu*) rai, fikra na hukmu hizi katika mageuzi, kubadilika na ijtihadi; na hakika ya ijtihadi hino katika mitagaa na msingi na je Uislamu huikiri au la. Kama kuifahamu hulazimisha somo la nafsiya ya Ummah inayoshuhudia rai, fikra na hukmu za Uislamu zimezama katika dunia hino inapoishi, na zile zinazotekelezwa juu yake katika nidhamu ya maisha na nidhamu ya utawala kupitia panga, njama na mali.

Kadhalika kuifahamu hulazimisha maarifa ya mwelekeo wa Ummah yenyewe kwa ujumla, na mtazamo wake kwa nidhamu zinazotabikisha zenye kuhatarisha Uislamu wake kupotea na zinazowaangamiza katika janga la dhiki na balaa (*ti'asa*). Kisha maarifa ya mwelekeo wa wasomi katika Ummah na vipi wanavyokubali nidhamu fisidifu inayotawazwa juu yake, na kama mashtaka yanachangamshwa ndani yao; na maarifa ya vipi huathiriwa na matamanio/hongo na vitisho, na vipi wanafuata (*insiyaq*) matamanio haya na kunyenyekea kwao kwa vitisho hivi.

Kisha maarifa ya kikundi cha kichama nafsi yake, na kuhakikisha kwamba inamiliki hisia ilionyolewa (*murhaf*), fikra ya kindani, ikhlasi safi na kwamba (*ijraat*) yanayotokea katika mujtama yasidhoofishe imani yake kwa Uislamu na Sheria zake; na kwamba yote yanayotokea ya hongo/matamanio, vitisho na ugaidi, ufadhili na mitihani, haiathiri chochote ndani yake. Kisha kuhakikisha kwamba kikundi hichi kinahifadhi thamani (*qaym*) zake za kibafsi kikamilifu na kwamba eneo lake na imani isalimike na iishibishe na fikra za Kiislamu za kindani, kutabanni maslahi za watu amma, na hisia yake kwa jukumu lake—yote haye yawe kamili kwa kiasi ya kwamba mfumo iwe katika ngome iliohifadhika juu ya yote yatakayo ifikia katika dhulma (*'isf*), maovu, shida na ugaidi. Kisha kuhakikisha kwamba kikosi hichi kime makinisha nia yake kubeba jukumu pamoja na kupima kwake kila natija na kujitayarisha kuyabeba.

Na usomi huu katika harakati za kijamii ni ya kitarekhe na ya hali ilivyo, inayoongoza kwa hakika ya sera ya chama cha kimfumo kwa sifa yake kama harakati ya kijamii, na kuhakikisha kwamba imekamilisha shuruti zake ikienda katika njia ya kimaumbile. Hata ikionekana ukombo au ikionekana kwamba darasa zahitaji marekebisho katika muundo (*jihaz*) au

katika sera au ukali katika mapambano, hufuatwa mbinu ambayo itaidhaminia kutekeleza ujumbe wake kuamsha Ummah, na kuijaalia kubebwa kwa watu na umma zote.
Chama itakwenda kisera kwa muundo sahihi kwa njia ifuatayo:-

1).Kuongoka kwa mfumo kwa mtu mwenye fikra na hisia ya hali ya juu. Itaingiliana naye mpaka itakuwa safi kabisa (*yatabalawwar*) kwake na kuwa wazi. Hapo patapatikanwa kiini cha kwanza kivitendo wala haitachelewa mpaka izidi kiini hichi kipolepole ili wapatikane watu wengine ambawo watakuwa viini. Watawasiliana baadhi yao mawasiliano kamilifu na mfumo mpaka waundwe halaqa ya mwanzo ya kikundi cha kichama (uongozi wa chama). Hakuna budi kuwa mfumo kipekee si nyengine kuwa ni msingi (*mihwar*) ya kikundi baina watu hawa, na pia kuwa peke yake ndio nguvu iliowavuta kuizunguka.

2).Hino halaqa ya kwanza itakuwa—kikawaida—wachache kiidadi, wapolepole kiharakati mwanzo kwa sababu pamoja na kuwa inazungumza kwa hisia ya mujtama inayoishi ndani yake, mazungumzo yake ni kwa maneno na maana tofauti na waliozowea watu kuyasikia. Na itakuwa na fahamu mpya tofauti na fahamu ziliotawala katika mujtama hata kama inazungumza kwa hisia yake. Kwa hivyo halaqa hino itakuwa kama mgeni kwa mujtama wala hawatovutiwa watukwake mwanzo ila mwenye hisia nguvu mpaka kiwango inapatikana ndani yake uwezekano wa kuvutiwa kwa (*maghnetis*) ya mfumo ilioko kiwiliwili katika halaqa ya kwanzo.

3).Itakuwa fikra ya halaqa hino ya kwanza (uongozi)—kikawaida—ya kindani, na twarika yake katika mwamko ya kimisingi yaani kuanza kwa mzizi. Kwa hivyo itatukuka halaqa hino juu ya hali mbaya inaoishi ndani yake Ummah. Na halaqa hino itaruka juu katika mazingara ya juu na kuona hali inayotakikana kuigurisha Umma kwayo yaani kuona maisha mapya inayotakikana kuigurisha Umma kwayo kama inavyoona njia itakayo fuata kubadilisha hali hino. Kwa hivyo huona nyuma ya saqafu kwa wakati aghlabu ya mujtama inayoishi ndani yake huona yaliyo mbele yao, na kwa hukmu ya kushikana kwao na hali mbaya ilioko ndani yake hushindwa kuruka juu na huwa vigumu kufahamu mbadiliko wa hali ufahamu sahihi. Kwa sababu mujtama uliodidimia itakuwa fikra yake katika (*bidaa*) yake, na (*yastamid suwar*) zake zote juu ya hali yake kisha hupima kila kitu juu yao kipimo jumla makosa na hujiunda nafsi yake juu yake inayofanya manufaa yake kuzunguka juu ya hali ilivyo.

Amma halaqa ya kwanzo, itakuwa kwa fikra yake imevuka marhala ya (*bidai*) na itakwenda kwa njia ya ukamilifu. Itafanya hali ilivyo kituo cha kufikiri ili kuigeuza kulingana na mfumo si chimbuko ya fikra kwa kufanya mfumo izunguke hali ilivyo. Kwa hivyo itajaribu kubadilisha

hali ilivyo na kuiunda na kuifanya inyenyekee kwa lengo lake ili kuifanya izunguke mfumo inayoiamini si kufanya mfumo kuzunguka hali ilivyo. Kwa hayo kutakuwa tofauti baina ya mujtama na halaqa ya kwanzo katika kufahamu mtazamo wa kimaisha juu ya uhai inayohitaji mkurubiano.

**1.** Fikra ya halaqa ya kwanza (uongozi) inategemea qaida thabiti ambayo ni kwamba hakuna budi fikra iungane na kitendo, na kwamba fikra na kitendo hakuna budi ziwe kwa ajili ya lengo maalumu zinazoilenga. Kwa hayo hupatikana ndani yake kutokea mfumo ndani yake, na kutokea fikra kutegemea qaida—hupatikana kutokea haya mazingara thabiti ya imani inayosaidia kuifanya hali ilivyo kunyenyekea na kuibadilisha kwa sababu fikra haiundwi kwa muundo ya yanayotokea bali huunda yanayatokea kwa muundo wake. Tofauti na mujtama iliodidimia isiokuwa na qaida kwa fikra yake kwa sababu kwa mjumuiko wake haijui lengo inayotenda kwa ajili yake, na lengo kwa watu wake binafsi ni za haraka za kibinafsi. Kwa hayo haipatikani kwake mazingara ya imani basi hulazimika kujiunda kwa mujibu ya yanayomzingira si kuyaunda kwa muundo wake binafsi. Kutoka hapa hutokea mgongano baina halaqa ya kwanza ya chama na mujtama inayoishi ndani yake mwanzoni.

**2.** Kwa sababu katika jukumu la halaqa ya kwanzo ya chama (uongozi) ni kuzalisha mazingara ya imani ambayo italazimisha twarika katika kufikiri, ni juu yake kuzalisha harakati za kimaksudi ili kukuwa kwake kukuwa kiharaka na kusafisha mazingara yake kikamilifu mpaka ibuniwe mwili wake wa chama ujenzi wa kuaminika na kwa haraka ya hali ya juu. Na kubadilika—kwa maendeleo ya haraka—kutoka halaqa ya kichama kuwa kikundi cha kichama kasha kuwa chama kamili kwa kulazimisha nafsi yake juu ya mujtama kwa njia iwe na athari juu ya mujtama si yenye kuathiriwa.

**3.** Hizi harakati za maksudi zitakuwa kwa masomo ya busara juu ya mujtama, watu na mazingara, na kwa kuchunga kimsingi isiingie katika umbo la chama kiungo (*'unsur*) fasidi na kusitokea kosa katika kuunda chombo katika vyombo vya chama ambayo itakuwa kikundi kwa mujibu wake mpaka isielekee kwa mtazamo usio mtazamo sahihi na mpaka chama kisigawanyike vipande viwili katika nafsi yake.

**4.** Lazima iwe aqeeda makini thabiti, na thaqafa ya chama ilioiva, ndio mfungamano baina wanachama wa chama na iwe ndio kanuni inayopeleka jamii ya chama wala si kanuni ya idara ilioandikwa katika karatasi. Twarika ya kutilia nguvu hino aqeeda na thaqafa ni kusoma na fikra ile kuunda akili khasa na ili fikra iwe iweungana na hisia. Na hakuna budi kubakia mazingara ya imani (*mukhayyam*) juu ya chama kwa

uzima wake mpaka iwe (*jami'*) katika chama vitu viwili yaani moyo na akili. Kwa hayo hakuna budi kwa imani kwa mfumo hata moyo uanze kujumuisha baina watu binafsi wa chama, kisha somo la kindani la mfumo na kuihifadhi, (*istidhar*) na kuifahamu ili kuunda mfungamano wa pili iwe ni akili. Kwa hayo chama itaandaliwa maandilizi sahihi na itakuwa mfungamano makini yenye nguvu inaoiwezesha kusimama imara mbele ya kila mtetemeko.

**5.** Uongozi wa chama (halaqa ya kwanza ya chama) hufanana na engine ya mtambo kwa sura moja na hutofautiana nayo kwa sura nyengine. Sura ya kufanana nayo ni: Engine ya mtambo ya petroli kwa mfano ina nishati ya moto inaozaliwa kutokamana na moto na 'benzene' katika harakati ya ki-engine. Hino nishati ya kimoto huzalisha 'pressure' katika hewa na hino 'pressure' husukuma (*dhira'*) ambayo ndio yenye kupeleka na ndio inaolazimisha harakati yake juu ya viungo vyengine na chombo kinazunguka. Kwa hayo kuwepo moto na benzene na harakati ya ki-engine ndio msingi kwa sababu ndio huzalisha nishati ya moto inaoleta 'pressure' na 'pressure' hino hulazimisha harakati yake juu ya viungo viliobakia na huzungusha engine. Basi ikisimama engine husimama viungo vyote. Basi hakuna budi kuwepo moto na benzene na harakati ya ki-engine mpaka izunguke engine na kuzunguka vyombo vyote. Kadhalika uongozi wa chama (halaqa ya kwanza ya chama) kwa sababu fikra ndani yake ni kama moto, na hisia katika watu wenye busara katika uongozi ni kama benzene, na mtu ambaye hisia yake huathirika na fikra ndio harakati ya ki-engine. Kwa hivyo pindi fikra inawasiliana na hisia katika mtu huleta nishati ya harara, na uongozi inasukumwa kwa harakati. Na harakati yake hino hulazimisha viungo vyote viliobakia vya chama katika watu binafsi, halaqa, kamati za eneo na nyenginezo, basi huathiriwa na harara yake na huanza harakati na zote kuzunguka mzunguko wa chombo. Hapa huanza mwenendo wa chama na harakati na huanza mzunguko kuwa katika muundo wake.

Kwa hivyo hakuna budi kutokea nishati ya harara kutoka uongozi kwa mabakio ya viungo vya chama mpaka izunguke kama hakuna budi kuweko harakati ya ki-engine ili chombo izunguke. Hino ni sura ya kufanana baina engine ya mtambo na uongozi wa chama. Kwa havyo ni lazima viongozi wa chama wafahamu sura hino na kuendeleza mawasiliano na harakati zao na mabakio ya viungo vya chama ili harara ya uongozi iathiri wote. Basi wakiwasiliana mara kadha na waone mabakio ya wanachama na kamati havijachangamka ili wakizichangamsha, wasife moyo na wajue kwa hino ni jambo la maumbile kwa sababu chombo hakizunguki ila engine ikizunguka na kutuma harara ndani yake.

Lakini uongozi (halaqa ya kwanza ya chama) haiwi ni yenye kuathiri kwa kulazimisha harakati juu ya chama kama (*dhira'*) inavyolazimisha harakati yake juu ya mabakio ya vyombo katika engine ya mtambo, bali harakati yake sampuli hino ni katika mwanzo wa jambo tu. Amma baada mwenendo wa chama, haiwi kama hivi. Basi kwa sura hino uongozi (halaqa ya kwanza ya chama) hukhalifu engine ya mtambo kwa sababu engine ya mtambo hubakia daima ndio yenye kuchamgamsha chombo lakini uongozi ni engine ya kimujtama sio engine ya mtambo. Na wanachama wa chama, halaqa zake na kamati zake za ki-eneo, ni wanadamu si chuma; ndani yao iko uhai na huathiriwa na harara ya uongozi yaani huathiriwa na harara ya mfumo inayojitia kiwiliwili ndani ya uongozi (halaqa ya kwanza ya chama). Kwa hivyo baada wamefahamu fikra na kuwasiliana kwao na harara ya uongozi ya chama huwa sehemu ya engine. Na huwa wakati huo kuwepo tu harakati ya uongozi, kama matunda wa nishati ya harara, inatuma harakati katika chama chote kimaumbile kwa sababu—nayo ni engine ya kimujtama—itakuwa muungo mmoja wa kififikra ilioenea katika chama kizima. Wakati huo haitobakia uongozi peke yake ndio inaobeba harakati ya ki-engine bali—kwa kuwa kwake na kukamilishwa muundo wa chama—itakuwa chama kizima hubeba harakati ya ki-engine. Kwa hivyo haihitaji mwenendo wa chama harakati ya uongozi wala kutuma harara yake, bali mfumo utapeleka wanachama wa chama na kupelea halaqa zake na kamati za kieneo mwenendo wa kichombo pasina haja ya haraka ya uongozi kwa sababuharakra ya kila sehemu imetokamana ndani yake na kutoka muungo mmoja wa kififikra ilioenea katika chama na kuwepo na mawasiliano ya kimaumbile baina sehemu hizi.

**6.** Chama cha kimfumo itaenda katika marhala tatu mpaka ianze kutabikisha mfumo wake katika mujtama wake:-

Mwanzo: Marhala ya darasa na kusoma ili kuunda thaqafa ya kichama.

Pili: Marhala ya maingiliano na mujtama inaoishi ndani yake mpaka mfumo iwe desturi jumuiyya (*'ura 'amma*) inaotokamana na busara na jamii nzima ichukue kuwa ni mfumo wake mpaka iitetee kijamii. Na katika marhala hino hunza mapambano baina ya Ummah na waliosimama kama vizuizi mbele ya kutabikisha mfumo miongoni kama ukoloni na iliowaweka mbele yao katika kikundi cha kutawala, watu wa giza na waliofitinishwa na thaqafa geni, kwa sababu huchukua imechukua mfumo ni mfumo wake na chama ni kiongozi wake.

Tatu: Marhala ya kuchukua mifunguo ya utawala kwa njia ya Umma kikamilifu mpaka utawala uchukuliwa kama twarika ya kutabikisha mfumo juu ya Umma. Katika marhala hino itaanza upande wa kivitendo katika chama katika maisha na itabakia upande wa ulinganizi kwa mfumo

ni kazi msingi wa serikali na chama kwa sababu mfumo ni ujume inayobebwa na Ummah na serikali.

**7.** Amma marhala ya kwanza, hino ni marhala ya kimsingi…nayo ni kuchukua watu wote binafsi katika Ummah kisawa kwa kuwa tupu na kila thaqafa na kuanza kumsomesha thaqafa yake mwenye kutaka kuwa mwanachama katika chama. Na kuchukua mujtama mzima ni madrasa ya chama mpaka chama kitoe kwa muda mfupi uwezekanayo kikundi kitakacho weza kuwasiliana na jamii na kuingiliana nao.

Lakini lazima ijulikane kwamba kusomesha thaqafa si taalimu na hutofautiana na skuli tofauti kamili. Kwa hivyo ni lazima thaqafa ya halaqa ipelekwe kwa kuchukuliwa mfumo ndio mwalimu na kwamba elimu na thaqafa inaochukuliwa imefupishwa kwa mfumo, na yanaolazimika kupitia mambo ya maisha, na huchukuliwa kutendwa nao moja kwa moja katika mambo ya maisha.

Kwa hivyo hakuna budi kuwa thaqafi ni ya kivitendo yaani kuchukuliwa kutenda nao katika maisha, na hukuna budi kuwekwa kizuizi kizito baina akili na upande wa kimasomo mpaka isielekee thaqafa ya kichama mwelekeo wa thafaqa ya ki-elimu ya skuli.

**8.** Chama ni kikundi kilichosimama juu ya fikra na twarika yaani juu ya mfumo waliouamini watu wake. Na huwa ni msimamizi juu ya fikra na hisia ya mujtama kuipeleka katika harakati ya kupanda juu, na huja kati baina ya kuporomoka katika fikra na hisia. Ni madrasa ya Umma ambayo huisomesha thaqafa na kuisukuma katika mambo ya maisha ya kiulimwengu. Nayo ni madrasa ya kikweli wala madrasa/skuli nyengine hazijitoshelezi nayo hata zikitofautika, kuzidi na kuwa pana. Lakini kuna tofauti baina chama na skuli ambao ni lazima ifahamike. Tofauti honi ni wazi katika nukta tofauti kama:-

**a)** Skuli, hata barnamij (syllabus) yake ziwe sahihi hazidhamini kuamsha Umma pasina kuwepo chama kinachosimama kama madrasa yake kwa sababu ni katika maumbile ya skuli—kadri inavyojikomboa—ni lazima iwe na utaratibu wa kupangwa basi husimama kwa muundo fulani na kuchukua sifa fulani na kwa hivyo kupoteza uwezekano kujiunda kufuata muundo wa hali ilivyo. Zikitaka kujiunda zinahitaji kazi ngumu na wakati fulani mpaka utokee marekebisho, na uandazi wake huwa kwa msingi thabiti usioundwa (upya).

**b)** Chama ikisimama juu ya barnamij sahihi itakuwa ndani yake:

1—Uhai basi itakuwa,
2—Mabadiliko mpaka igure kutoka hali mpaka hali,

3—Harakati basi itaweza kuenda katika kila upande wa mujtama na katika kila sehemu ya biladi.
4—Hisia basi huhisi na kufahamu kila kinachotokea katika mujtama kuathiri ndani yake.

Na uandazi wake utakuwa kwa msingi wa muundo wa uhai na hisia basi ndani yake ni mabadiliko ya kudumu na mageuzi yasiomalizika, kwa sababu huenda na uhai na muundo wake ili kuinda na mazingara ya imani na kubadilisha hali ilivyo ya kuirekebisha kwa mujibu wa mfumo.

**c)** Skuli husimama kusomesha thaqafa mtu binafsi, (*tahdhib*) na kumsomesha kwa kumchukua kama mtu binafsi maalumu. Na juu ya kuwa kwake jamii ndogo lakini ni ya kiubinafsi katika mtazamo wake wa kusomesha basi natija zake huwa za kibinafsi si za kijamii. Hata tukisema mji una wakaazi kumi elfu na ina skuli inazokusanya wanafunzi elfu, hazitoweza kuzalisha mwamko wowote wa kijamii katika mji.

**d)** Chama husimama kulea jamii na kuisomesha thaqafa yake kwa sifa yake ya jamii moja pasina kujali watu binafsi wake. Haiwatizami hawa watu binafsi walioko ndani yake kwa sifa yao kuwa watu binafsi maalumu bali huwatizama kwa sifa yao kuwa sehemu ya jamii. Huwasomesha thaqara kijamii kusuluhisha sehemu za jamii si watu binafsi wao. Kwa hayo huwa natija za chama za kijamii si za kinafsi. Lau twasema kwamba jamii katika eneo ina wakaazi milioni na ndani yake iko chama ambao wanachama wake ni mia, inaweza kuzalisha mwamko katika eneo hino inaowashinda skuli kadri zinavyotumia juhudi na kupita zama na kukhitimisha wanafunzi.

**e)** Chama husimama kutayarisha mtu binafsi kuathiri jamii anayoishi ndani yake wala hatoweza kuathiri ili kisehemu kwa sababu yeye huchukua sehemu ya kihisia ilio na athari dhaifu katika kuamsha fikra.

**f)** Chama kinasimama kutayarisha jamii ili kumuathiri mtu binafsi nayo (jamii) yaweza kuathiri kikamilifu kwa sababu hisia yake ni yenye nguvu, ya kuamsha, inayoweza kuamsha fikra. Kwa hivyo athari yake kwa watu binafsi ni yenye nguvu na huamsha ndani yao mwako kwa juhudi ndogo na muda mfupi zaidi kwa sababu inayoamsha fikra ni hisia na kwa kuingiliana kwao hutokea harakati ya mwamko.
Hufupishwa tofauti baina chama na skuli kwa nukta tatu:-

**a)** Skuli ni yenye kupangwa (*ratabiyya*) isioweza kujiunda ilhali chama ni yenye kugeuka/kuendelea (*mutatawir*) si yenye kufungwa na mpangilio na huweza kujiunda katika uhai basi huiunda kwa mazingara yake ya imani.

**b)** Skuli humsomesha thaqafa mtu binafsi ili aathiri katika jamii basi natija zake ni za kibinafsi ilhali chama husomesha jamii thaqafa ili imuathiri mtu binafsi basi natija zake ni za kijamii.

**c)** Skuli hutayarisha sehemu ya kihisia katika mtu binafsi ili aathiri hisia za jamii basi hawezi kuiathiri na hushindwa kuamsha fikra yake ilhali chama hutayarisha hisia kamilifu katika jamii ili iathiri hisia za watu binafsi basi huweza kuwaathiri na huweza kuamsha fikra zao kikamilifu.

**9.** Katika marhala hino hapana budi kuwa na fahamu daima kwamba mujtama kwa uzima wake ndio skuli kubwa ya chama pamoja na ufahamu wa daima wa tofauti kubwa baina skuli na chama katika halaqa zake za kusomesha thaqafa.

Amma kufahamu kwamba mujtama kwa uzima wake ndio skuli ya chama huu ni kwa sababu kazi ya chama katika wakati huu ni kuamsha itikadi kweli na kuunda fahamu sahihi. Na hayo hayatotokea ila kwa amali ya kusoma thaqafa ambayo mfumo wa chama ndio mwalimu na thaqafa yake ndio mada ya kusomwa, na mfumo huu ya thaqafa yake inawakilishwa na iliowaingilia kiwiliwili mfumo basi wao ndio waalimu moja kwa moja wa mujtama na itakuwa kamati la eneo na halaqa zake ni klasi zake na itakuwa mujtama mzima ndio madrasa. Hino amali ya kusome thaqafa hulazimisha wanachama katika chama na wanaotabanni fahamu zake masomo makini na ufahamu sahihi, kukumbuka thaqafa ya kichama kila wakati, wakihifadhi katiba yake na hukmu muhimu na qaida jumla ilizozitabanni. Hino huhitaji amali ya kusoma thaqafa. Kwa hayo hakuna budi kutia hamu kwa upande huu pamoja na kila mwenye kuingia katika chama, pasina kujali kuwa amesoma thaqafa ya chuo kikuu au ya skuli ya kimsingi au ana uweza wa kusoma thaqafa. Kila madharau katika thaqafa na mtu yeyote humbakisha mtu binafsi huyu kuwa nje ya boma la chama hata kama ajinasibisha nayo na huenda kuzalisha madhara katika muundo jumla.

Hakuna budi kuweka vizuizi nzito baina kitendo na chama katika marhala hino kabla kuwepo ndani yake watu waliosoma thaqafa ya kichama kwa hivyo marhala hino ni marhala ya kusoma thaqafa si mambo mengine.

Amma kufahamu tofauti baina skuli na chama katika thaqafa, hino ili isigeuke thaqafa ya kichama kuwa thaqafa ya kiskuli basi chama kipoteze uweza wake kuathiri. Kwa hivyo hakuna budi kuwekwa kizuizi kizito baina wanachama wa chama na upande wa kimasomo (ya kiskuli) katika thaqafa ya kichama na itambuliwe kuwa thaqafa ya kichama ni ya kugeuza ufahamu na kuitenda katika nyanja za maisha na kubeba uongozi wa fikra kwa Ummah. Haijuzu kumsukuma mwanafunzi kwa upande wa

kimasomo (ya kiskuli) na ikiwa ana haja ya kimasomo basi mahala pake ni skuli si chama. Ni hatari kusukumwa na thaqafa kuelekea upande wa kimasomo kwa sababu hino hupokonya sifa ya kutenda na kuchelewesha kugura kwa marhali ya pili katika marhala.

**10.** Marhala ya pili ni marhala ya maingiliano na Umma na ndio inayosuhubiwa na mapambano. Huchuliwa kuwa ni marhala makini na kufaulu ndani yake ni dalii ya usawa wa kuundwa chama. Na kuangamia ndani yake ni dalili kuwa na upungufu ndani yake ambayo lazima itengenezwe. Hino hubuniwa juu ya marhala kabla yake kwa hivyo kufaulu katika marhala ya kwanzo ni sharti msingi ya kufaulu katika marhala ya pili. Lakini kufaulu tu katika marhala kwa usomi wa thaqafa haitoshi peke yake kufaulu katika marhala hino, bali hakuna budi kuwa kufaulu kithaqafa yajulikana kwa watu yaani watu wajue kwamba kuna da'wa na wajue kutoka mwanachama kwamba yeye anabeba da'wa kama hakuna budi kuwa roho ya kijamii imeundwa ilipoundwa halaqa kithaqafa, kuwasaliana wanachama katika mujtama wanaoishi ndani yake na majaribio yao kuiathiri mpaka wanapogura kwa marhala ya pili huwa maandazi ya kijamii ipo basi husahilika kwao kuingiliana na Umma.

**11.** Mwanachama wa chama haguri kutoka marhala ya kusoma thaqafa kwenda marhala ya maingiliano mpaka amekhitimu kithaqafa, kukhitimu inayomfanya shakhsiyya wa Kiislamu, akili yake ikilingana na nafsiyya yake. Asema :( saaw) *"Hajaamini mmoja wenu mpaka hawa zake hufuata nilichokuja nacho."* Na watu wajue kutoka kwake kwamba ywabeba da'wa ya Kiislamu, na mielekeo ya kijamii yamekuwa na kudhihirika na nguvu ndani yake kwa kuweko kwake katika halaqa na kuingiliana na mujtamaa kiasa ya kwamba kujitenga imeng'olewa ndani yale kwa sababu kujitenga ni mtangamano wa uoga na kukata tamaa, hakuna budi kuing'oa kutoka watu binafsi na mujtama.

**12.** Chama itagura kutoka marhala ya thaqafa kwenda marhala ya maingiliano kugura kimaumbile kwa kiasi ya kwamba lau ingelitaka kugura kabla wakati wake haingeweza. Hino ni kwa sababu marhala ya thaqafa hukamilisha ndani yake nukta ya kuanzilia kwa sababu thaqafa hufanya mfumo kuingia kiwiliwili ndani ya watu na hufanya mujtama kuhisi da'wah na mfumo hisia wazi. Pindi inapotimia mfumo kuwaingilia kiwiliwili watu yaani kuipanda katika nafsi zao na kutimia pamoja nayo mujtama kuhisi mfumo, da'wa itakuwa imevuka nukta ya kuanzilia basi itakuwa haina budi kugura kufikia nukta ya kujitokeza. Ili ianza chama mwenendo katika nukta ya kujitokeza, haina budi kuanza kukhutubia Ummah. Na ili ianze kuwakhutubia lazima ianze na kujaribu kuwakhutubia mwanzo mpaka ikafaulu katika kujaribu hivi ndipo itabadilika kwa kukhutubia moja kwa moja. Kujaribu kukhutubia itakuwa

kupitia thaqafa ya kimsingi katika halaqa, kupitia thaqafa ya kijamii kwa watu katika kila mahali inaowezekana, kufichua mipango ya ukoloni na kutabanni maslahi ya Ummah. Basi ikifaulu kwa katika mambo haya manne pamoja itageuka kukhutubia Ummah na kuguria nukta ya kujitokeza kimaumbile. Itakuwa kujitokeza kwake hivi kufikia nukta ya kujitokeza ndio inayoigurisha kimaumbile kutoka marhala ya kwanzo, ambayo ni marhala ya thaqafa, kufikia marhala ya maingiliano, na kuifanya kuanza maingiliano na Umma kwa wakati wake kuanza kimaumbile.

**13.** Maingiliano haya na Ummah ni dharura kufaulu chama katika kazi yake kwa sababu kadri wanavyozidi wanachama wa chama katika Ummah lakini hawaingiliani nayo, hawaoweza kutekeleza kazi peke yao, kadri itakavyo kuwa nguvu yao, ila Ummah ikifuatana nao. Wala hawatoweza kuiongoza Ummah kufanya kazi wala hawatofuatana na wao ila wakiingiliana nao na wafaulu katika maingiliano haya. Si maana ya kuingiliana na Ummah kuweza kwao kuwakusanya watu kuwazingira bali maana ya kuingiliana ni kufahamisha Ummah mfumo wa chama ili iwe mfumo wao kwa sababu asli ya mfumo—nao ni Uislamu—ipo katika Ummah kwa sababu hisia za Ummah hugeuka kuwa fikra inayokuwa wazi katika kikosi pwekee ambao chama inaundwa kutoka kwao. Ikawa qaida ya hisia (nayo ni fikra na kutenda kwa ajili ya lengo) ni msemo hakika wa mfumo. Kwa hivyo itakuwa mfumo (yaani Uislamu) ndio hisia ndani ya Ummah, na chama itakuwa ni msemaji wa hisia hino. Basi ikiwa fasihi katika kusema, wazi katika lugha, mkweli katika (*lahja*) Ummah itafahamu kiharaka na kuingiliana na chama na itachukuliwa Ummah kwa uzima wake kuwa ndio chama. Kikosi pwekee itabeba uongozi wa harakati kupitia kikundi cha kichama, harakati hiyo ambao Ummah itafuatana nayo kwa uongozi wa chama kuelekea marhala ya tatu nayo ni kutabikisha mfumo utabikishaji wa kimapinduzi, kupitia njia ya utawala ambao hichi kikundi cha kichama kitakiwala, kwa kuichukua twarika pekee kutekeleza fikra yaani kuichukua sehemu ya mfumo.

Lakini kuna matatizo mengi yanosimama usoni mwa maingiliano huu, basi hakuna budi kujua maumbile yao ili kufanya kazi kuyazidi nguvu. Muhimu zaidi katika matatizo haya mengi ni:-

**a)** Kugongana mfumo na nidhamu inaotabikishwa katika mujtama.

Mfumo wa chama ndio mfumo mpya wa maisha ukifananishwa na mujtama wa kileo, nayo hugongana na nidhamu inaotabikishwa katika mujtama huu ambao kikosi cha kutawala huhukumu watu nao. Kwa hivyo itaona khatari juu yake, na umbo lake, kutoka mfumo huu basi haina budi kusimama usoni mwake na kuipiga vita kwa mbinu tofauti: uvumi dhidi yake, kufukuza wabebaji da’wa na kutumia mbinu za

kinguvu. Kwa hivyo ni juu ya wabebaji da'wa—nao hutenda kuingiliana na Umma kwa da'wa ya mfumo wake—kujikinga na maudhia kwa kila wanaoweza na kupinga uvumi mpotofu kwa kusherehesha mfumo wao na kubeba kila dhiki katika njia hino.

**b)** Na katika matatizo ni ikhtilafu ya thaqafa.

Ipo katika mujtama thaqafa tofauti, na ipo katika Ummah fikra zisiofanana lakini ina hisia moja. Thaqafa nyingi, makhsusan thaqafa za kikoloni, zitakuwa misemo ya kugongana na hisia hino ilhali thaqafa ya mfumo, yaani thaqafa ya Kiislamu, itakuwa msemo kweli wa hisia ya Ummah. Lakini rai amma ya kithaqafa na manhaj ya thaqafa katika skuli na (*ma'ahid*) na kila mahala la kithaqafa inayokwenda kulingana na thaqafa geni. Kadhalika yaliobakia katika harakati za kisiasa na thaqafa huenda kulingana na thaqafa geni. Kwa hivyo chama hiana budi katika thaqafa yake kuingia katika marhala ya mapambano na thaqafa na fikra nyengine mpaka hudhirika kwa Ummah msemo kweli wa hisia na (*shu'ur*) zake ili ifuatane nayo. Hwa hayo hakuna budi kuwepo katika marhala hino mgongano baina chama katika thaqafa na fikra yake na isiokuwa yeye katika thaqafa na fikra nyengine. Mgongano huu ni baina watoto wa Ummah, kwa hivyo marhala haichukui (njia ya) mjadala bure bali jamaa ya chama itafuata njia ya kuchora laini (*khatt*) ilionyoka upande wa laini ilio kombo wala haitoingia mjadala bure kabisa ili isifikishe kwa ubinafsi inaoleta upofu na kuziba masikio mbele ya uhakika. Bali hushereheshwa fikra za chama na hubainishwa urongo wa fikra nyengine, na ubatili katika thaqafa nyengine na hatari ilioko katika matunda yake. Wakati huo Ummah itajiepusha nazo na kuelekea mwelekeo wa thaqafa na fikra ya chama, bali watu wake pia watajiepusha nazo baada kudhihirika kwao urongo wake ikiwa walikuwa miongoni mwa wasafi wenye busara mukhlisina. Lakini hino amali ni katika amali ngumu zaidi kwa chama, kwa hivyo kuzalisha maingiliano na Ummah katika eneo iliokathirika ndani yake thaqafa geni ni nguvu zaidi kushinda maeneo iliopunguka ndani yake thaqafa hino. Na uwezekano wa mwamko katika maeneo iliopunguka ndani yake kiasa cha watu waliosomesha thaqafa geni ni kubwa zaidi kushinda maenedo inaopanda kiasi hichi. Kwa hivyo ni juu ya chama kuwa na busara makini ya jamii inaofanya maingiliano nao kufuata njia inaofaa nao.

**c)** Katika matatizo ni kuwepo watu wanaofuata hali ilivyo (pragmatists) katika Umma.

Vipo vikosi viwili vinaowakilisha hali ilivyo katika Umma kwa sababu ya thaqafa geni na kuenezwa sumu geni na ujinga.

Amma kikosi cha kwanza hicho ni kikosi cha kufuata hali ilivyo wanaolingania kwa hali ilivyo na kurudhika na hali ilivyo na kusalimu

amri kwayo kama jambo la lazima kwa sababu kikosi hichi huchukua hali ilivyo kama chimbuko ya fikra yake na huchukua kwayo suluhisho za matatizo yake. Njia ya kushinda tatizo hino ni kujaribu kupanua akili na wao katika uchunguzi mpaka waone na kufahamu kwamba mazingara huchukuliwa kama kituo cha kufikiri ili kuigeuza ili kwa hayo waweze kuregea nyuma katika fikra zao.

Amma kikosi cha pili hicho ndicho kikosi cha watu wa giza kinacho kataa kuishi katika nuru kwa sababu wamezowea maisha katika giza, mambo yasio na maana na fikra duni na wameswibiwa na maradhi ya uvivu wa kimwili na akili na wameshikamana na ya zamani waliowapata nao wazee wao kwa sababu tu ni ya zamani. Basi hawa ni wenye kufuata mambo yalivyo kikweli kwa sababu wao ni jinsi ya hali ilivyo kifikra. Kwa hivyo wana haja ya kupewa nafasi (*mu'anat*) kubwa zaidi. Njia ya kushinda tatizo hino ni kujaribu kuwasomesha thaqafa na kufanya bidii kusahihisha ufahamu wao.

**d)** Na katika matatizo inaosimama mbele ya da'wa ni watu kushikamana na maslahi yao.

Hiyo ni kwa sababu mawanadamu ashikana na maslahi yake ya kibinafsi, kazi yake ya kila siku na hushikana wakati huo huo na mfumo. Inaweza kuonekana kwamba maslahi haya yanagongana na da'wa kwa mfumo kwa hivyo hujaribu kuleta muafaqa baina yao. Kushinda tatizo hino ni lazima juu ya kila mwenye kuamani mfumo kufanya da'wa na chama kuwa ni msingi inaozunguka juu yake maslahi yake ya kibinafsi. Haijuzu kushughulika na kazi yeyote inaogongana na da'wa wala katika kazi yeyote inaomsahaulisha da'wa na kumregesha nyuma nayo. Kwa hivyo itakuwa imenukuliwa da'wa kutoka kuzunguka juu ya maslahi kufanya maslahi yazunguke juu ya (*mihwar*) yake (da'wh).

**e)** Na katika matatizo inaosimama mbele ya da'wa ni tatizo la kujitolea katika mambo ya maisha ya dunia katika mali, biashara na mifano yake katika njia ya Uislamu na kubeba da'wa yake. Kushinda tatizo hino muumini hukumbushwa kwamba Allah amenunua kutoka waumini nafsi na mali zao ili awape Pepo. Ukumbusho huu watosheleza na huachwa na khiyari ya kujitolea kwa mambo haya wala halazimishwi chochote. Aliandika (ass) barua kwa Abdullah bin Jahsh pindi alipomtuma kuongoza kikosi kuwatizama maQureshi Nakhla, baina Makka na Taif, na ikaja katika barua hino: "Wala usimlazimishe sahibu wako kufuatana na wewe, na endelea na amri yangu katika wanao kufuata."

**f)** Inaweza kudhaniwa kwamba katika matatizo ni tofauti za ki-mji katika mujtama, na hiyo ni kuwa Ummah itakuwa na mazingara ya ki-miji tofauti na mazingara ya vijiji, na tofauti na mazingara ya kibedui; na

kuwa madaniyya katika miji tofauti na ilioko katika vijiji na hiyo katika vijiji kuwa tofauti na ilioko katika maeneo ya kibedui na (*khaym*). Hino yaweza kuleta madhania kwa chama kwamba tofauti hino katika sura za kimadaniyya fikra ya kutofautisha katika kusomesha thaqafa au katika mwelekeo wa kimfumo. Hino ni kitu cha hatari kubwa zaidi kwa sababu Ummah, kadri inavyo tofautika ndani yake sura za kimadaniyya, ni Umma mmoja, hisia yake ni mmoja na mfumo wake ni mmoja kwa hivyo itakuwa da'wa kwake ni moja pasina kutofautisha baina miji na vijiji na itakuwa kazi ya maingiliano pamoja nayo ni moja.

**14.** Itatokea kwa chama katika marhala hino (marhala ya maingiliano na Umma) hatari mbili: hatari ya kimfumo (yaani kwa mfumo) na hatara ya kitabaka.

Amma hatari ya kimfumo, hino itakuja kutoka mwelekeo wa jamii na hamu kuitikia matlaba yake ya (*mulha*) ya kisasa, na itakuja kwa mabakio yaliopo katika rai za jamii kuzidi nguvu juu ya fikra ya kichama.

Hiyo ni kwa sababu pindi chama kinapo jitumbukiza katika (*ghimar*) ya maisha katika mujtama, itawasiliana na jumuiyya ili kuingiliana nao na kuwaongoza. Na wakati huo huo ambao chama kitakuwa kinajiandaa na mfumo wake, itakuwa jumuiyya imekusanya ndani yake mgongano mwa fikra za kuregelea nyuma za kale, urathi kutoka karne iliopita, na fikra geni hatari na kuigiza mkafiri mkoloni. Pindi chama kinapotekeleza amaliyya ya maingiliano na jumiyya, itawaandaa na rai na fikra za chama, na kufanya juhudi kusahihisha fahamu zao na kuamsha aqeeda ya Kiislamu ndano yao, na kuunda mazingara ya kweli na *'urf amm* sawa kupitia fahamu za chama. Hino yahitaji da'wa na 'propaganda' hata ikusanye Ummah pamoja nayo kwa msingi wa mfumo, kwa sura inayotia nguvu imani ya mfumo katika Umma na kuamsha ndani yake imani juu ya fahamu za chama, kuitukuza na kuihishimu, na kuibeba kuwa tayari kutwii na kutenda. Wakati huo itakuwa wajibu wa chama ni kuzidisha mashababu wake waumini na wanaotegemewa miongoni mwa Ummah ili wawe wasimamizi wa amri yake kama maafisa katika jeshi. Chama ikifaulu kwa maingiliano katika marhala hino, itaongoza Ummah kwa lengo inayotaka ndani ya mipaka ya mfumo, na itakuwa na amani kutoka gari la moshi kupinduka (*khatt*).

Amma chama ikiongoza jumuiyya kabla kukamilisha maingiliano nawo, na kabla kuwepo wai amm katika Ummah, uongozi wake itakuwa si kwa hukmu na fikra za mfumo bali kwa kupima yale yanaokasirisha Ummah, kususia hisia zake na kwa kuonyesha kwamba matlaba yake yako karibu mkononi.

Lakini jumuiyya hino haijatolewa ndani yake katika hali hino hisia zake za mwanzo za kizalendo, kikabila, kiroho wa kikasisi, na itakuwa hali ya kijamii imeathiriwa nazo, basi itadhihirika ndani yake ada duni kama utaifa na umadhehebu, na fikra za kale kama utengamano na uhuru, na (*na'arat*) fisidifu kama ukabila wa rangi na ujamii, basi itaanza mgongano baina yake na chama kwa sababu itakuwa yalazimisha kwa nafsi yake matlaba yasiolingana na mfumo. Na itaita miito ya kudhuru ya kisasa, kuhamasika na matlaba haya, na kuzidi mchangamko wake kuyahakikisha; na itadhihirika ndani yake (*na'arat*) nyingi. Katika hali hino itakuwa msimamo wa chama baina moto mbili: mojawapo ni kujitolea kwa hasira za Ummah na kuikasirikia (*nuqma*), na kuvunja kilichojenga ya utawala juu ya jamii. Ya pili ni kujitolea kujitenga mfumo wake na kulegea kwake, na kila moja katika haya mawili ni hatari kwake. Basi ni juu ya watu wa chama ikiwa jambo linagongana baina ya jumuiyya na mfumo kushikamana na mfumo, hata ikijitolea kwa kusarikiwa na Ummah kwa sababu hino ni hasari ya kiwakati, na kuthubutu kwao juu ya mfumo itaweregeshea imani ya Ummah. Na wajitahadharishe na kukhalifu mfumo na kujitenga na msingi wake kipimo cha unyoa kwa sababu hiyo ndio uhai wa chama na ndio inayodhamini kubakia kwake. Ili kujikinga na msimamo mgumu kama huu, na kujitenga na hatari kama hino, ni juu ya chama kujitahidi ku(*saqiyy*) Ummah mfumo wake na kuhifadhi uwazi wa fikra na fahamu za chama, na kutenda kazi ili kubakisha mazingara yake kutawala juu ya Umma. Hino itasahilishwa na kutia hamu ya kuvukia mipaka juu ya wakati wa kusomesha thaqafa, na kuzidi kutia hamu kwa kusomesha thaqafi jamii, kufanya bidii ya kimakini kufichua njama na ukoloni, na kudumu katika kuchunga Ummah na maslahi yake, na kuyayusha kikamilifu baina mfumo na chama, kudumu kuchunguza fikra za chama na fahamu zake ili zibakie safi, na kujitolea kijuhudi inayoweza kwa haya yote kadri hii itaikalifisha kijuhudi na hamu.

Amma hatari ya kitabaka, hino yaweza kupenya kwa watu wa chama si kwa Ummah. Hino ni kwa sababu pindi chama kinapowakilisha Ummah au wengi wao, kitakuwa na nafasi ya juu na makao ya kutukuzwa, na kupendwa kamili kutoka kwa Ummah na watu wa juu. Hino yaweza kuamsha ghururi katika nafasi basi watu wa chama wajione wao ndio wakuu kushinda Ummah na kwamba kazi yao ni uongozi na kazi ya Ummah ni kuongozwa. Wakati huo watajiinua juu ya watu binafsi wa Ummah au baadhi yao pasina kujali. Haya yakikiririwa Ummah itahisi kwamba chama ni tabaka nyengine tofauti, na chama kitahisi utabaka huu. Hisia hino ni mwanzo wa njia ya kuangamia chama kwa sababu hamu ya chama ya imani ya watu kawaida wa Ummah itadhoofika na imani ya jumuiyya kwa chama itadhoofika; wakati huo Ummah itaanza

kujitenga na chama. Pindi Ummah inajitenga na chama itakuwa (chama) imeangamia, na itahitaji kujitolea juhudi mara nyingi hata kuregesha imani hino. Kwa hivyo ni lazima juu ya watu wa chama kama watu kawaida wa Ummah wala wasihisi kinafsi ila kwamba wao ni watumishi wa Ummah, na kwamba majukumu yao ya kichama ni kutumikia Ummah kwa sababu hino itakuwa hifdhi kwao na kuwanufaisha si tu kwa kudumu imani ya jumuiyya kwao wao lakini pia kuwanufaisha katika marhala ya tatu wanapotawala utawala ili kutekeleza mfumo. Basi watabakia—kama viongozi—watumishi wa Ummah ili wawe sahali kutekeleza mfumo.

**15.** Marhala ya tatu, nayo ni marhala ya kufikia kwa utawala.
Chama itafikia kwa utawala kupitia njia ya Ummah na vitendo vya kutafuta nusra, na itatekeleza mfumo kwa wakati moja; na hino ndio inayoitwa twarika ya kimapinduzi. Twarika hino haikubali kushiriki kivipande katika utawala bali huchukua utawala kikamilifu na kuichukua twarika kutabikisha mfumo wala si lengo. Mfumo wa Uislamu hutekelezwa kimapinduzi wala haikubali twarika ya kupanda daraja (*tadarruj*) hata dhurufu ziwe aina gani.

Pindi mfumo inatabikishwa kikamilifu katika kila nyanja, ni juu yake kubeba da'wa ya Kiislamu, basi huwekwa katika 'budget' ya kiserikali mlango maalumu wa da'wa na 'propaganda' na hutawaliwa usimamizi wa da'wa hino kwa upande wa kiserikali au upande wa kichama kulingana na dhurufu zinavyohitaji. Pasina kujali chama kufuikia utawala, itabakia chama ikiendelea na muundo wake ukisimama, sawa wawe wanachama wake katika vita vya utawala ama la. Itachukuliwa utawala khatua ya kwanzo ya kivitendo kutekeleza mufmo wa chama katika serikali, na kujitolea kuitekeleza katika kila sehemu ya ulimwengu.

Hizo ndizo khatua ambazo chama itafuata katika nyanja za maisha ili kunukulu fikra kufikia marhala ya kivitendo. Kwa msemo mwengino, ili kunukulu mfumo kufikia nyanja za maisha kwa kuregesha maisha ya Kiislamu ili kuleta mwamko kwa mujtama na kubeba da'wa kwa ulimwengu. Wakati huo chama itaanza marhala ya kivitendo nayo ndio marhali ambao iliundwa kwa ajali yake. Kwa hivyo chama ndio dhamana ya kihakika kusimamisha serikali ya Kiislamu, kubakia kwake, kutabikishwa Uislamu na kutabikishwa kwake vizuri, kudumu utabikishaji juu na kubeba da'wa kwa ulimwengu. Kwa sababu baada ya kusimamisha serikali itakuwa mlinzi juu yake, mwenye kuihisabu, ikiongoza Ummah katika kuijadili; na wakatu huo huo itakuwa ikibeba da'wa ya Uislamu katika biladi za Kiislamu na nyenginezo katika mabakio ya sehemu ya ulimwengu.